# NYARAKA 3



COMIC BIBLE
SOCIETY

Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2023

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.


MWANDISHI WA WAHEBRANIA HAJULIKANI LAKINI TUNAJUA KUWA BARUA HII ILIANDIKIWA JAMII YA WAYAHUDI...
WAEBRANIA
...WENGINE WALIOAMINI NA WENGINE AMBAO BADO HAWAKUMWAMINI YESU KRISTO.
BARUA HII INALINGANISHA NJIA ZA ZAMANI ZA MUNGU KUPITIA MAKUHANI NA KAFARA NA NJIA BORA. WAUMINI SASA WANA NJIA MOJA KWA MOJA KWA MUNGU KUPITIA KRISTO.
MUNGU ALIZUNGUMZA NA MABABU ZETU KUPITIA MANABII KWENYE MAONO, NDOTO, NA HATA ANA KWA ANA - LAKINI SASA ANAZUNGUMZA NASI KUPITIA MWANAWE."
YESU NI MKUU ZAIDI YA MALAIKA NA JINA LAKE NI KUU KULIKO MAJINA NA NAFASI ZA MALAIKA."
MALAIKA WAKE NI WAJUMBE WA KIROHO WALIOTUMWA KUWASAIDIA WANAOFAA KUPOKEA WOKOVU WAKE.


KWA KUWA UJUMBE WA MALAIKA ULIPATIKANA KUWA WA KWELI NA WATU WALIADHIBIWA KWA KUTOTII - NI NINI KINACHOTUFANYA TUNAWEZA KUEPUKA TUSIPOJALI WOKOVU HUU MKUU?
NA ILIKUWA SAWA KWAMBA MUNGU ALIYEUMBA KILA KITU KWA UTAKATIFU WAKE, ALIKUBALI YESU ATESEKE, KWANI KWA KUFANYA HIVI ALIKUWA ALETA UMATI MKUU MBINGUNI.
"KUPITIA KUTII KWAKE, YESU ALIKUWA MFANO MUFTI KWA WAUMINI."
YEYE YESU ALIKUWA MWILI NA DAMU KAMA SISI - KWANI KWA KUFA KAMA BINADAMU PEKE YAKE NDIO ANGEVUNJA NGUVU ZA IBILISI.
HAKUJA KAMA MALAIKA ILA KAMA MWANADAMU-MYAHUDI. ILIBIDI AWE KAMA NDUGU ZAKE, ILI AWE KUHANI WETU MKUU MWENYE REHEMA NA MUAMINIFU.
KWA KUWA YEYE MWENYEWE ASHAPITIA MATESO NA MAJARIBU ANAJUA ILIVYO TUNAPOTESEKA NA KUJARIBIWA NA ANA UWEZO WA KUTUPA USAIDIZI WA AJABU.


VILE AMBAVYO MUSA ALIMTUMIKIA KWA UAMINIFU, YESU ALIKUWA MUAMINIFU KWA MUNGU ALIYEMCHAGUA KAMA KUHANI MKUU.
LAKINI YESU ANA UTUKUFU MWINGI ZAIDI YA MUSA, KAMA VILE MTU ANAYEJENGA NYUMBA APATAVYO SIFA ZAIDI YA NYUMBA YAKE.
TUTAHADHARI TUNAPOSIKIA SAUTI YAKE TUSIACHE MIOYO YETU IGEUKE DHIDI YAKE, KAMA WATU WA ISRAELI WALIOKUFA JANGWANI MAANAKE HAWAKUPATANISHA NA IMANI.
AHADI YA MUNGU BADO IPO-ATAKA KUTUOKOA-KAMA VILE WAKATI WA MUSA.
LAKINI UJUMBE HAUKUWAFAA ISRAELI KWA SABABU HAKUUWEKA PAMOJA NA IMANI.
HUU NDIO WAKATI WAKUMUAMINI MUNGU - MSIKAZE MIOYO YENU WALIVYOFANYA.
KWANI CHOCHOTE ASEMACHO MUNGU NI KIKALI KULIKO KISU KIKALI ZAIDI, CHAKATA HADI MAWAZO YETU YA NDANI KABISA NA HAMU ZETU - KUFICHUA NAFSI YETU TULIVYO HASA.
KWA KUWA YESU, KUHANI WETU MKUU, AMEENDA MBINGUNI NA ANAELEWA UNYONGE WETU - WACHA TUJE KWA KITI CHA ENZI CHA MUNGU NA UJASIRI KUPATA REHEMA NA NEEMA.


KUHANI MKUU WA KIYAHUDI NI MTU TU KAMA MWENGINE YEYOTE, LAKINI ACHAGULIWA KUZUNGUMZA KWA NIABA YA WATU WOTE KATIKA SHUGHULI ZAO NA MUNGU.
HAKUNA AWEZAYE KUWA KUHANI MKUU KWA SABABU ANATAKA - LAZIMA ACHAGULIWE NA MUNGU.
NDIO MAANA KRISTO HAKUJICHAGUA KWA CHEO CHA KUWA KUHANI MKUU - ALICHAGULIWA NA MUNGU.
MUNGU ALIMUAMBIA, "MWANANGU, LEO NIMEKUPA SIFA."
TUWACHE KUPITIA MAFUNZO YALE YALE YA KWANZA KUMHUSU KRISTO.
TUSONGE MBELE KWA MAWAZO MAKUU NA KUKOMAA KWA MAWAZO YETU.
MUNGU AMETUAHIDI NA MUNGU HANA UWEZO WA KUDANGANYA.
TUMAINI HILI LINALOHAKIKISHA KUOKOKA KWETU LINATIA NANGA ROHO ZETU, NA KUTUUNGANISHA NA MUNGU NYUMA YA PAZIA ZA MBINGUNI AMBAPO KRISTO AMETANGULIA KUTUTETEA KAMA KUHANI WETU MKUU.


MELKIZEDEKI ALIKUWA MFALME WA MJI WA SALEMU NA PIA KUHANI MKUU WA MUNGU ALIYE JUU ZAIDI.
IBRAHIMU ALIGAWA SEHEMU YA KUMI YA VITU VYOTE ALIVYOSHINDA KATIKA VITA KWA MUNGU KUPITIA MELKIZEDEKI - NAYE MELKIZEDEKI AKAMBARIKI.
LAKINI MUNGU ATAKAPOTUMA AINA MPYA YA KUHANI, SHERIA YAKE LAZIMA IBADILIKE KUIRUHUSU.
KRISTO HAKUWA KUHANI NA MAHITAJI YA KALE ILA KWA MSINGI WA NGUVU ZINAZOTOKA KWA UHAI USIO NA MWISHO.
YESU AISHI MILELE NA ANEDELEA KUWA KUHANI KWA HIYO AKUNA MWENGINE ANAYEHITAJIKA NA AWEZA KUOKOA KABISA WOTE WANAOKUJA KWA MUNGU KUPITIA KWAKE.
NI KUHANI MKUU TUNAYEHITAJI HASA - NI MTAKATIFU NA HANA DOSARI.
HAHITAJI KAFARA YA DAMU YA WANYAMA KILA SIKU - KWANI ALIMALIZA KAFARA ZOTE, KWA MARA MOJA, ALIPOJITOA KAFARA MSALABANI.


KRISTO, KUHANI WETU MKUU, ANAHUDUMU HEKALUNI MBINGUNI, MAHALI PA KWELI PA IBADA PALIPOJENGWA NA BWANA NA SIO MIKONO YA BINADAMU.
KWANI KWENYE MFUMO WA ZAMANI ZAWADI NA KAFARA ZILITOLEWA, LAKINI HAZIKUWEZA KUSAFISHA MIOYO YA WATU WALIOZILETA.
KANUNI HIZI ZILIBAKI MPAKA KRISTO ALIPOKUJA NA NJIA YA MUNGU MPYA NA BORA ZAIDI.
KAFARA ANAYOTOA NI BORA KULIKO ZILIZOTOLEWA NA MAKUHANI WA ULIMWENGUNI.
AGANO LA KALE HALIKUFANYA KAZI. KAMA INGEFANYA, KAZI HAKUNGEKUWA NA HAJA YA KUIBADILISHA NA NYENGINE.
KRISTO NI KUHANI MKUU WA MFUMO HUU BORA TULIO NAO SASA.
ALIINGIA PATAKATIFU ZAIDI, AKANYUNYIZA DAMU YAKE MWENYEWE KATIKA KITI CHA REHEMA.
BINADAMU WAMEKUSUDIWA KUFA MARA MOJA, KISHA BAADA YA HIVYO KUHUKUMIWA NA MUNGU.
ATAKUJA TENA KULETA WOKOVU KWA WOTE WALE WANAOMNGOJEA KWA HAMU NA SUBIRA.
1879
1934
FATHER
HUSBAND


MFUMO WA ZAMANI WA SHERIA ZA KIYAHUDI HAUNGEWEZA KUWAOKOA WALIOISHI CHINI YA SHERIA HIZO.
KAFARA ZILE ZA KILA MWAKA ZILIWAKUMBUSHA DHAMBI ZAO, KWANI HAIWEZEKANI DAMU YA NG'OMBE DUME NA MBUZI KUONDOA DHAMBI KWA HAKIKA.
NDIO MAANA KRSITO ALISEMA, "EH MUNGU, DAMU YA NG'OMBE DUME NA MBUZI HAIKURIDHISHI, KWA HIYO UMETAYARISHA MWILI HUU WANGU KUNIWEKA KAMA KAFARA JUU YA MADHABABHU YAKO."
"NIMEKUJA KUFANYA NIA YAKO, KUWEKA MAISHA YANGU, VILE AMBAVYO MAANDIKO YALISEMA NITAFANYA."
KWA YOTE ALIYOTUFANYIA, TUSHINDANE KWA KUWA WENYE KUSAIDIA NA WAKARIMU KWA WENGINE NA KWA KUFANYA WEMA.
MSIPUUZE MIKUTANO YA KANISA, BALI MTIANE MOYO KILA UCHAO.
YEYOTE AKIFANYA DHAMBI KUSUDI KWA KUMKATAA MWOKOZI BAADA YA KUUJUA UKWELI WA MSAMAHA, DHAMBI HII HAIJAFINIKWA NA KIFO CHA KRISTO.
HAKUTAKUWA NA CHOCHOTE KUTAZAMIA ILA ADHABU MABAYA YA HASIRA YA KUTISHA YA MUNGU, ITAKAYOMALIZA MAADUI WAKE.


IMANI NI UHAKIKA WA UAMINIU KUWA TUNACHOKITAKA KITAFANYIKA NA UHAKIKA TUNACHOTUMAINI KINATUNGOJA - HATA KAMA HATUIONI.
WATU WA MUNGU ENZI ZA ZAMANI WALIJULIKANA KWA IMANI YAO.
KWA IMANI HABILI ALIMTII MUNGU NA KULETA DHABIHU ILIYOMFURAHISHA MUNGU KULIKO ALIYITOA KAINI.
HENOKA ALIMUAMINI MUNGU NA KUHAMISHWA MBINGUNI BILA KUFA.
KWA IMANI YAKOBO, ALIPOKUWA MZEE AKIFA ALIMBARIKI KILA MMOJA WA WANA WA YUSUFU.
WAZAZI WA MUSA WALIKUWA NA IMANI NA KUMFICHA KINYUME CHA AMRI YA FARAO.
MUSA ALIKATAA KUCHUKULIWA KIFALME BALI ALICHAGUA KUSHIRIKI MATESO NA WATU WA MUNGU BADALA YA KUTENDA DHAMBI.


NUHU ALISIKIA ONYO LA MUNGU NA KUJENGA SAFINA KABLA DALILI YOYOTE YA MAFURIKO.
IBRAHIMU ALIAMINI MUNGU ALIPOMUAMBIA AONDOKE NYUMBANI AENDE KWENGINE.
SARA ALIKUWA NA IMANI NA KUWA MAMA LICHA YA UMRI WAKE MZEE.
WENGINE WALIMUAMINI MUNGU WAKASHINDA VITA, KUPINDUA UFALME, KUTAWALA VYEMA NA KUPATA MUNGU ALICHOWAAHIDI.
WENGINE WALIPIGWA, WENGINE WAKATUPWA GEREZANI, WENGINE WAKAFA KWA KUPIGWA MAWE NA HATA KUKATWA MARA MBILI KWA MSUMENO, BALI HAWAKUWAHI KUIKANA IMANI YAO.


KWA KUWA UMATI HUU WA WAUMINI UNATUTAZAMA, TUVUE CHOCHOTE KINACHOUPUNGUZA MWENDO WETU, HASA ZILE DHAMBI AMBAZO ZINATUKWAZA; NA TUKIMBIE MBIO ALIZOTUANDALIA MUNGU.
WEKA MTAZAMO WAKO KWAKE YESU, KIONGOZI WETU NA MWALIMU WETU.
ALIKUA TAYARI KUFA KIFO CHA AIBU MSALABANI KWA SABABU YA FURAHA ALIYOJUA ATAKUWA NAYO BAADAYE - NA SASA ANAKAA MAHALI PA HESHIMA KWA KITI CHA ENZI CHA MUNGU.
BABA ZETU WA DUNIANI WALITUADHIBU KWA NJIA BORA WALIOIJUA LAKINI ADHABU YA MUNGU IKO SAWA NA NZURI KWETU WAKATI WOTE, ILI TUSHIRIKI KATIKA UTAKATIFU WAKE.
MATOKEO YAKE NI KUKUA KWETU KWA NEEMA NA TABIA.
TAHADHARI MTU YEYOTE ASIHUSIKE KATIKA DHAMBI YA NGONO AMA KUTOJALI KAMA ESAU ALIYEUZA HAKI YAKE KAMA MWANA WA KWANZA KWA MLO MMOJA.
INGAWA ESAU ALISIHI KUREGESHEWA LAKINI YALIKWISHAFANYIKA.
DANCERS
NA SASA MUNGU WA AMANI ALIYEMLETA TENA KUTOKA MAUTI BWANA WETU YESU KRISTO, AWATAYARISHE NA KILA MNACHOHITAJI KUTIMIZA MAPENZI YAKE.
KWAKE UWE UTUKUFU MILELE NA MILELE. AMINA.


YAKOBO
BARUA YA YAKOBO ILIANDIKWA B.K. 44-49, KUKIFANYA KITABU CHA KWANZA KATIKA KANUNI YA AGANO JIPYA.
MWANDISHI NI YAKOBO - NDUGU WA KAMBO WA YESU NA NDUGU YAKE YUDA.
PIA ALIITWA YAKOBO MPENDA HAKI KWA SABABU ALIPENDA SANA MAISHA YA UTAKATIFU NA KWA WAFUASI WA KRISTO KUWA NA UTIIFU.
BARUA KUTIKA KWA YAKOBO ILILENGA MUUMINI WA KIYAHUDI ALIYEKUWA AMETAPAKAA KUTOKANA NA MATESO, INAWEZEKANA CHINI YA HERODE AGRIPA I.
"KWA KABLA KUMI NA MBILI WALIOTAWANYIKA."
"HESABUNI YA KUWA NI FURAHA TUPU MKIANGUKIA KATIKA MAJARIBU MBALIMBALI - MKIJUA YA KUWA MAJARIBU YA IMANI YENU HULETA SABURI."
"KWANI SABURI YENU IKIKAMILIKA, BASI MTAKUWA TAYARI KWA LOLOTE, WENYE TABIA ILIYOKOMAA, WAKAMILIFU NA WATIMILIFU."
YAKOBO 1:1-4


"KAMA MWATAKA KUJUA KILE MUNGU ATAKA MFANYE, MUULIZENI, NA ATWAAMBIA KWA FURAHA, KWANI ATAWAPA HEKIMA WOTE WATAKAOMUULIZA"
"LAKINI ULIZENI KWA IMANI KWANI AKILI YENYE SHAKA ITAKUWA ISOTULIA KAMA WIMBI LINALOPEPERUSHWA NA UPEPO."
"MKRISTO ALIYE CHINI NA AFURAHI - KWANI YU MKUU KWA USO WA BWANA."
"LAKINI ALIYE TAJIRI AFURAHI KWANI KARIBUNI ATAKWENDA, KAMA UA LINALONYAUKA KWA JUA KALI LA HARI."
"HERI NI MTU ASTAHIMILIYE MAJARIBU KWANI ATAPOKEA TAJI."
"WAKATI MTU ANAPOJARIBIWA SIO MUNGU ANAYEMJARIBU - KWANI MUNGU HAMJARIBU YEYOTE."
CASINO
Venus
POT
ENTER
"NI VIZURI KUWA MWEPESI WA KUSIKILIZA, MPOLE WA KUZUNGUMZA NA MPOLE WA KUKASIRIKA; KWANI HASIRA YA BINADAMU HAILETI MAISHA YA UTAKATIFU MUNGU ALIYOPANGIA,
U MPUMBAVU!
"MTU YEYOTE ANAYEJIDHANIA MKRISTO WALA HAUDHIBITI ULIMI WAKE ANAJIDANGANYA TU, NA DINI YAKE HAIFAI."
"DINI ANAYOIKUBALI MUNGU NI ILE INAYOWAANGALIA MAYATIMA NA WAJANE NA KUJIWEKA KUTOKA KUHARIBIWA NA DUNI."
YAKOBO 1:5-27


"MNAWEZAJE KUSEMA NYINYI NI WA BWANA YESU KRISTO KAMA MNAPENDELEA MATAJIRI NA KUWADHARAU MASIKINI."
"NI DHAMBI MKIWAPENDELEA MATAJIRI NA KUWASIFU MNO."
"MUNGU AMEWACHAGUA WATU MASIKINI KUWA MATAJIRI KATIKA IMANI."
"HAMTAMBUI YA KUWA NI MATAJIRI WANAOWAPELEKA KORTINI NA WANAOMCHEKA YESU KRISTO?"
"KUNA HAJA GANI KUSEMA KUWA MNA IMANI KAMA HAUIONYESHI KWA KUWASAIDIA WENGINE. IMANI AINA HIYO ITAMUOKOA YEYOTE?"
"IMANI ISIYOONEKANA NA MATENDO MEMA SIO IMANI HATA KIDOGO-IMEKUFA NA HAINA MAANA."
"KUNA WENGINE KATI YENU AMBAO WANASEMA "KUAMINI TU" INATOSHA?"
"MNAAMINI MUNGU MMOJA? BASI MAPEPO PIA WANAAMINI - NA WANATETEMEKA!"
"RAHABU, KAHABA, ALIOKOLEWA KWA SABABU YA ALICHOKIFANYA ALIPOWAFICHA WAJUMBE NA KUWATUMA KWA USALAMA NA NJIA TOFAUTI."
"VILE VILE AMBAVYO MWILI UMEKUFA WAKATI HAKUNA ROHO BASI IMANI IMEKUFA KAMA SIO ILE INAYOTOA MATENDO MEMA."


"USIWE MWEPESI KUWAAMBIA WENGINE MAKOSA YAO KWANI SOTE TWAFANYA MAKOSA MENGI."
"KAMA YEYOTE AWEZA KUDHIBITI ULIMI WAKE INADHIBITISHA ANAJIDHIBITI KWA KILA NJIA NYENGINE."
"TUNAWEZA KUMFANYA FARASI MKUBWA AGEUKE KWA KUTUMIA LIJAMU NA USKANI MDOGO WAFANYA MELI KUBWA KUGEUKA KILA NAHODHA ANAPOTAKA KUIGEUZA."
"KWA HIYO PIA ULIMI NI KITU KIDOGO LAKINI WAWEZA KUWA NA UHARIBIFU MKUU."
"BINADAMU WAMEWAFUGA KILA AINA YA WANYAMA NA NDEGE LAKINI HAKUNA ALIYEUFUGA ULIMI."
"NA KWA HIYO, KUBARIKI NA KULAANI KWATOKA KWA KINYWA KIMOJA - HAKIKA HII SI SAWA."
"KAMA UNA HEKIMA ISHI MAISHA YA WEMA THABITI ILI MATENDO MEMA PEKE YAKE YATAKUTOKA."
"KWANI WIVU NA UBINAFSI SIO HEKIMA YA MUNGU. VITU HIVYO NI VYA ULIMWENGU, SIO VYA KIROHO, VINAHAMASISHWA NA IBILISI."
"LAKINI HEKIMA INAYOTOKA MBINGUNI NI SAFI KWANZA NA IMEJAA UPOLE MTULIVU. NA INAPENDA AMANI NA HESHIMA. IMEJAA REHEMA NA MATENDO MEMA."
YAKOBO 3


"NI NINI KINACHOSABABISHA UGOMVI NA VITA - SIO KWA SABABU YA TAMAA ZA KIOVU KATI YENU?"
75% CLEARANCE
"HAMNA KWA SABABU HAMULIZI MUNGU - NA MKIMUULIZA, MWATAKA KWA RAHA ZENU."
"HAMJAGUNDU KUWA KUFANYA URAFIKI NA TAMAA ZA KIOVU ZA ULIMWENGU HUU-KUNAWAFANYA ADUI WA MUNGU."
SMITH
"MUNGU ANAPATIANA NGUVU KWA WALIONYENYEKEA LAKINI ANAWAPINGA WENYE MAJIVUNO NA MARINGO."
"KWA HIYO JITOENI KWA UNYENYEKEVU KWA MUNGU. MPINGE SHETANI NA ATAWAKIMBIA."
"NA MKIMKARIBIA MUNGU, NAYE ATAWAKARIBIA."
"NYINYI MNAOSEMA, 'LEO AMA KESHO KUTAFUNGUKA BIASHARA YENYE FAIDA.'"
"INAFAA MSEME, "MUNGU AKIPENDA TUTAISHI NA KUFANYA HIVI AMA VILE."


"TAZAMENI ENYI MATAJIRI - SASA NDIO WAKATI WA KUANZA KULIA NA GUNA KWA SABABU YA SHIDA ZA KUTISHA ZILIZO MBEE YENU."
"MUMETUMIA MIAKA YENU MKIRIDHISHA NAFSI YENU KWA KILA NJIA NA SASA MIOYO YENU ILIYONONA I TAYARI KUCHINJWA."
"WAPENDWA, MSIAPE KWA MBINGU WALA KWA ARDHI WALA KITU CHENGINE CHOHOTE; SEMA TU NDIO AU LA ILI MSITENDE DHAMBI NA KULAANIWA KWA SABABU YAKE."
"KUNA MMOJA KATI YENU ANAYETESEKA - MUACHE AOMBE."
"WALIO NA SHUKRANI WAIMBE SIFA KWA BWANA."
"KUNA MMOJA ANAYEUGUA - MUACHE AWAITE WAZEE WA KANISA WAMUOMBEE NA KUMWALIA MAFUTA NA KUITA JINA LAKE BWANA AMPONYE."
"KIRI MAKISA YENU KWA WENZENU NA KUOMBEANA ILI MPONYWE."
"OMBI LA KWELI LA MTU MTAKATIFU LINA UWEZO MKUU NA MATOKEO YA AJABU."
"KAMA MTU YEYOTE ANAPOTEA KUTOKA KWA MUNGU NA MWENGIN AKAMSAIDIA KUELEWA UKWELI TENA - MTU HUYO ATAKUWA AMEOKOA ROHO YA KUTANGA KUTOKA KIFO NA KULETA MSAMAHA WA DHAMBI NYINGI."
HOLY BIBLE


MNAMO B.K. 64 MJI WA ROMA ULIUNGUA KATIKA MOTO MKUU - WARUMI WENGI WALIAMINI ILIFANYWA NA NERO KWA TAMAA YAKE KUJENGA.
WARUMI WENGI WALIUWAWA NA WENGI HAWAKUWA NA MAKAO.
NERO ALITAKA KUELEKEZA HASIRA ZA WATU WAKE...
ENEZA HABARI WAKRISTO NDIO WALIFANYA - KWANI, WANAFUNZA ULIMWENGU UTAISHA NA MOTO.
BASI, UKAANZA MDA WA MIAKA 200 YA MATESO DHIDI YA WAFUASI WA KRISTO.
MTUME PETERO ALITUMA BARUA HII KWA WAKRISTO WALIOTAPAKAA KUELEZA VILE AMBAVYO WAFUASI WA KRISTO WANAPASWA KUCHUKULIA CHUKI NA KUISHI ULIMWENGUNI.
"KWA WALIO TAWANYIKA PONTO, GALATIA, KAPADOKIA NA ASIA NA BITHINIA -MUNGU BABA ALIWACHAGUA ZAMANI NA ALIJUA MTAKUWA WANA WAKE."
"MAJARIBU HAYA NI YA KUJARIBU IMANI YENU, KUONA KAMA NI KUU NA SAFI."
"KAMA VILE MOTO UNAVYOSAFISHA DHAHABU-IMANI YENU NI YA THAMANI ZAIDI KWA MUNGU KULIKO DHAHABU."
"TAJI ZAIDI LA KUMUAMINI NI WOKOVU WA ROHO ZENU."
"WOKOVU HUU UNA KITU MANABII HAWAKUELEWA KWA KINA."


"ONDOENI HISIA ZENU ZA CHUKI."
"MALIZANENI NA UONGO NA WIVU NA KUWASENGENYA WENZENU."
"NJOONI KWA KRISTO AMBAYE NI JIWE LA MSINGI LILILO HAI AMBALO JUU YAKE MUNGU AJENGA."
"NA SASA MUMEKUWA MAWE YA KUJENGA YALIYO HAI YA MUNGU KUTUMIA KWA KUJENGA NYUMBA YAKE."
"AMEWACHAGUA MWENYEWE-MU MAKUHANI WA MFALME."
"KWA KUWA KWENU HASA NI MBINGUNI, NAWASIHI MUEPUKE TAMAA ZA KIOVU ZA ULIMWENGU HUU ZINAZOPIGANA DHIDI YA ROHO ZENU."
"NI MAPENZI YA MUNGU KUWA MAISHA YENU MEMA YAWANYAMAZISHE WAJINGA WANAOILAUMU INJILI."
"HESHIMU KILA MTU. MUOGOPE MUNGU NA IHESHIMU SERIKALI."
"KUTESEKA HUKU NI SEHEMU YA KAZI MLIYOPEWA NA MUNGU. KRISTO, AMBAYE ALITESEKA KWA AJILI YENU, NI MFANO WENU."
"ALIBEBA DHAMBI ZETU KWA MWILI WAKE MSALABANI ILI TUMALIZANE NA DHAMBI - KWANI VIDONDA VYAKE VIMEPONYA VYETU!"


"WAKE, WASTAHI MABWANA ZENU ILI KAMA HAWAAMINI WANAWEZA KUVUTIWA, SIO NA MANENO BALI NA MATENDO YA WAKE ZAO."
"MSIJIHUSISHE NA MAPAMBO YA NJE YA MAPAMBO, MAVAZI NA NYWELE - BALI MUWE WAREMBO KWA NDANI - NA ROHO YA UPOLE NA TULIVU."
"WAUME, YAZINGATIE MAHITAJI YA WAKE ZENU NA KUWAHESHIMU KAMA MRITHI WA UZIMA WA MILELE PAMOJA NANYI ILI KITU CHOCHOTE KISIKUZUIE KATIKA MAOMBI."
"KAMA WATAKA MAISHA MEMA YENYE FURAHA DHIBITI ULIMI WAKO, NA ULINDE MDOMO WAKO KUTOKANA NA KUSEMA UONGO."
"EPUKA MAOVU NA TENDA MEMA."


"KWA KUWA KRISTO ALITESEKA NA KUPITIA UCHUNGU LAZIMA MUWE NA MTAZAMO ALIOKUWA NAO - LAZIMA MUWE TAYARI KUTESEKA."
WHAACK
"MLIFANYA YA KUTOSHA HAPO AWALI KWA KUZINI, TAMAA, ULEVI, KUABUDU MIUNGU NA DHAMBI ZENGINE."
"MARAFIKI ZENU WA AWALI WATASHANGAA SANA MTAKAPOKUWA HAMNA HAMU YA KUUNGANA NAO, LAKINI LAZIMA WAPATANE NA YEYE ANAYEHUKUMU WALIO HAI NA WALIO KUFA."
"MWISHO WA DUNIA WAJA HIVI KARIBUNI. KWA HIYO MUWE WATU WANAOZINGATIA MAOMBI KWA BIDII."
"WAPENDWA, MSISHANGAE MNAPOPITIA MAJARIBU MAKALI KWANI SIO KITU KIGENI."
"BADALA YAKE, MUFURAHI KWA SABABU MU WASHIRIKI NA KRISTO KATIKA MATESO."
"FURAHIA UNAPOLAANIWA NA KUTUSIWA WA KUWA MKRISTO, KWANI ROHO WA MUNGU YUKO JUU YAKO KWA UTUKUFU MKUU."
"KAMA UNATESEKA KULINGANA NA MAPENZI YA MUNGU, ENDELEA KUFANYA KICHO SAWA NA UJIKABIDHI KWA MUNGU ALIYEKUUMBA."


"NA KWA WAZEE WA KANISA - MIMI PIA NI MZEE - NA NILIMUONA KRISTO AKIFA MSALABANI."
"LISHA NA KUJALI MIFUGO YA MUNGU KWA KUPENDA WALA SIO SHINGO UPANDE - SIO KWA KILE UTAKACHOPATA ILA KWA KUWA UNA HAMU KUMTUMIKIA BWANA."
"VIJANA FUATENI KWA UONGOZI WA WALIO WAZEE KUWALIKO NA MHUDUMU KWA ROHO NYENYEKEVU."
"NYENYEKEA CHINI YA MKONO MKUU WA MUNGU NA KWA WAKATI WAKE ATAKUINUA."
"TAHADHARI NA UVAMIZI KUTOKA KWA SHETANI - ANAZUNGUKA KAMA SIMBA ANAYENGURUMA AKITAFUTA WA KUMRARUARARUA."
"BAADA YA KUTESEKA KWA MDA KIDOGO MUNGU ATAWAPA UTUKUFU WA MILELE."
"ATAWAINUA NA KUWAWEKA MAHALI IMARA, NA KUWAFANYA WENYE NGUVU ZAIDI."
"KANISA HAPA ROMA LATUMA SALAMU."


ALIPOKUWA GEREZANI MDA MFUOI KABLA KIFO CHAKE MIKONONI MWA NERO, PETERO ALITUMA BARUA YA PILI.
ALIKUWA NA WASIWASI KUHUSU WALIMU WAONGO - UZUSHI WAO NA MAISHA YAO YA UASHERATI.
"WAPENDWA, FANYA BIDII KUONYESHA KUWA KWELI MU KATI YA WALE WALICHAGULIWA NA KUITWA NA MUNGU, KISHA HAMTAWAHI KUKWAZIKA AU KUANGUA."
WAPENDWA,
"LAKINI BWANA YESU KRISTO AMENIOYESHA KUWA SIKU ZANGU HAPA ULIMWENGUNI ZIMEHESABIWA NA NITAONDOKA HIVI KARIBUNI."
"BORA NIKO HAPA NINAKUSUDIA KUENDELEA KUTUMA UKUMBUSHO ILI MKUMBUKE MDA MREFU BAADA YANGU KUONDOKA."
KWANI HATUJAKUWA TUKIWAAMBIA HADITHI TULIPOWAELEZA UWEZO WA BWANA WETU YESU KRISTO NA KURUDI KWAKE."
"MACHO YANGU YAMEONA FAHAI NA UTUKUFU WAKE."


"LAKINI KULIKUWA NA MANABII WAONGO PIA, KATIKA SIKU HIZO, KAMA KUTAKAVYOKUWA NA WALIMU WAONGO KATI YENU."
"WALIMU HAWA KWA UROHO WAO WATAKUAMBIA CHOCHOTE KUPATA HELA ZAKO."
"KWANI MUNGU HAKUWAACHA MALAIKA WALIOTENDA DHAMBI LAKINI ALIWATUPA JEHANAM, NA MINYORORO KWA MAPANGO YA KUTISHA NA GIZA MPAKA SIKUA YA HUKUMU."
"NA HAKUWAACHA WATU WAKE WOWOTE WALIOISHI ENZI ZA KALE KABLA MAFURIKO - ISIPOKUWA NUHU NA JAMII YAKE YA WATU SABA."
"BWANA ALIMUOKOA LUTU KUTOKA SODOM KWA SABABU ALICHUKIZWA NA UOVU WA KUTISHA ALIOUONA UMEMZINGIRA SIKU HIYO."
"PIA, BWANA ANAWEZA KUTUOKOA KUTOKA MAJARIBU NA KUENDELEA KUADHIBU WASIO NA MUNGU MPAKA SIKU YA MWISHO YA HUKUMU.:
"WALIMU HAWA WAONGO HAWASHINDI WANYAMA - WATAANGAMIZWA PAMOJA NA MAPEPO NA NGUVU ZA JEHANAM KAMA MALIPO YA DHAMBI ZAO."
"WATU HAWA HAWANA MAANA KAMA CHEMCHEMI ZILIZIKAUKA MAJI, KUAHIDI MENGI BILA KUTOA CHOCHOTE; KAMA MAWINGU YANAYOSUKUMWA NA UPEPO WA DHORUBA HAWAKO IMARA."
"WAMEHUKUMIWA KWA SHIMO LA MILELE LA GIZA."
II PETERO 2


"NINGEPENDA KUWAKUMBUSHA KUWA KATIKA SIKU ZA MWISHO KUTAKUJA WADHIHAKI WATAKAOFANYA KILA KITU KIBAYA NA KUUCHEKA UKWELI."
"KUSUDI WANASAHAU KUWA MUNGU ALIANGAMIZA ULIMWENGU NA FURIKO KUU."
"LAKINI MSISAHAU HILI - KWA MUNGU SIKU NI KAMA MIAKA ELFU MOJA - NA MIAKA ELFU MOJA NI KAMA SIKU MOJA."
"SIKU YA BWANA INAKUJA KAMA MWIZI, NA MBINGU ZITAPITA NA SAUTI YA KUTISHA, NA MIILI YA MBINGUNI ITAPOTEA KWENYE MOTO."
"KWA KUWA KILA KITU KITAYEYUKA, TUNAFAA TUISHI MAISHA GANI YA KIUNGU!"
"MKUMBUKE BWANA." [1]
"LAKINI KUWA KWA NGUVU ZA KIROHO NA KUMJUA BORA ZAIDI BWANA WETU NA MWOKOZI YESU KRISTO."
"KWAKE UWE UTUKUFU NA HESHIMA YA FAHRI, SASA NA MILELE. KWA HERI."
[1] KULINGANA NA TAMADUNI PETERO ALIMUANGALI BIBI YAKE AKISULUBIWA NA AKAMTIA MOYO NA MANENO HAYA.


I, II, III YOHANA
YOHANA ALIKUWA MTUME WA MWISHO WA YESU KRISTO KUISHI NA ALIANDIKA BARUA HII KATI YA B.K. 90-95, KABAL TU YA KUTESWA CHINI YA MFALME DOMITIAN WA ROMA.
MTUME ALIANDIKA KWA KANISA YA ASIA NA KUZINGATIA HATUA ZA KWANZA ZA UGNOSTIKI. [1]
[1] UGNOSTIKI ULIFUNZA KUWA YESU HAKUFANYWA KUJA KIMWILI BALI ALIONEKANA KAMA AMBAYE ALIKUWA NA MWILI. WALIFUNZA MWILI ULIKUWA MUOVU TU, YAANI MTU ANGETENDA DHAMBI BILA KUATHIRI ROHO.
KRISTO ALIKUWA HAI ULIMWENGU ULIPOANZA - IJAPOKUWA NA MACHO YANGU NIMEMUONA NA KUMSIKIA.
NIMEMGUSA NA MIKONO YANGU MWENYEWE.
NI UJUMBE WA MUNGU WA UHAI.
"HUU NDIO UJUMBE MUNGU AMETUPA - MUNGU NI MWANGA NA NDANI YAKE HAKUNA GIZA KAMWE."
"TUKISEMA TU MARAFIKI WAKE LAKINI TUENDELEE KUISHI KATIKA DHAMBI, TUNADANGANYA."
I YOHANA 1






II YOHANA 2-3:2


"KAMA UNAFANYA KILICHO SAWA WAKATI WOTE NI KWA SABABU MKO WEMA KAMA YESU."
"LAKINI MKIENDELEA KUTENDA DHAMBI INAONYESHA MU WA SHETANI, ALIYETENDA DHAMBI TANGU MWANZO."
"KAMA TWAWAPENDA WAKRISTO WENGINE, INATHIBITISHA KWAMBA TUMEPEWA UZIMA WA MILELE."
"LAKINI MTU ASIYE NA UPENDO KWA WENGINE ANAELEKEA KWA KIFO CHA MILELE."
"KAMA DHAMIRA ZETU ZIKO SAWA TUNAWEZA KUJA KWA BWANA NA UHAKIKA NA KUPATA TUNACHOOMBA KWA SABABU TUNAMTII NA KUFANYA KINACHOMPENDEZA."
"MSIAMINI KILA KITU MNACHOSIKIA KWA SABABU MTU ANASEMA NI UJUMBE KUTOKA KWA MUNGU - JARIBU KWANZA."
"INAKUBAI KUWA YESU KRISTO, MWANA WA MUNGU ALIKUJA AKAWA NA MWILI WA MWANADAMU?
"HATUNA HAJA YA KUOGOPA - YESU ANATUPENDA KIKAMILIFU NA KUONDOA WOGA WA ANACHOWEZA KUTUFANYIA - HII NI KWA KUWA ALITUPENDA KWANZA."
"YEYOTE AKISEMA, 'NAMPENDA MUNGU,' LAKINI AMCHUKIE NDUGU YAKE, BASI ANADANGANYA."
"KAMA HUMPENDI NDUGU YAKO ALIYE MBELE YAKO, WAWEZAJE KUMPENDA MUNGU?"
I YOHANA 3:3-4:20


"KUMPENDA MUNGU INAMAANISHA KUFANYA ANACHOTUAMBIA NA SIO VIGUMU."
"MTOTO YEYOTE WA MUNGU ANAWEZA KUMTII, KUSHINDA TAMAA YA UOVU KWA KUMUAMINI KRISTO."
"NANI AWEZAYE KUSHINDA VITA HIVI ISIPOKUWA KWA KUAMINI KUWA YESU KWELI NI MWANA WA MUNGU?"
"MUNGU ALITHIBITISHA NA SAUTI KUTOKA MBINGUNI WAKATI WA KUBATIZWA KWA YESU NA PIA ALIPOKUWA MAUTINI."
"TUNAWAAMINI WATU WANAOTOA USHAHIDI KWA KORTI ZETU, BILA SHAKA TUNAWEZA KUAMINI CHOCHOTE ASEMACHO MUNGU."
"NA MUNGU ASEMA YESU NI MWANA WAKE."
"HAKUNA YEYOTE ALIYEUNGA JAMII YA MUNGU ANAYEZOEA KUTENDA DHAMBI, KWANI KRISTO ANAMSHIKILIA NA IBILISI HAWEZI KUMSHIKA."
"WATOTO WAPENDWA, JIEPUSHENI NA CHOCHOTE KINACHOWEZA KUCHUKUA MAHALIA PA MUNGU MIOYONI MWENU. AMINA."


BARUA YA PILI KUTOKA MTUME ALIYEBAKI HAI, YOHANA, ILIYOANDIKWA KARIBU B.K. 90-95.
MANDHARI - KUELEZA MIPAKA YA UKARIMU WA KIKRISTO.
MWILI WA YESU ULIONEKANA KUWA WA KWELI - ROHO YAKE ILIMUACHA KABLA KUSULUBIWA.
UGNOSTIKI[1] ULIKUWA UNAANZA NDANI YA KANISA, KAMA ALIVYOTABIRI PAULO.
[1] KUKATAA UBINADAMU WA KRISTO, KUSEMA KUWA MWILI NI MWOVU NA KUWA WAGNOSTIKI WALIKUWA NA UKWELI WA JUU.
KANISA YA AWALI ILIKUTANA KWA MANYUMBA NA WALIMU WAONGO WALIANZA KUWALAGHAI WAKRISTO WASIOKUWA NA HABARI - KUJA MAJUMBANI MWAO NA INJILI YA UONGO.
"KWA KUWA UKWELI UPO MIOYONI MWETU MILELE, MUNGU BABA NA YESU KRISTOMWANA WAKE WATATUBARIKI NA REHEMA KUU NA AMANI NYINGI, NA UKWELI NA UPENDO."
"SIVYO AMBAVYO NIMEFURAHI KUWAPATA BAADHI YA WANA WENU HAPA NA KUONA WANAISHI INAVYOPASWA - KUFUATA UKWELI NA KUTII AMRI YA MUNGU."


"NATAKA KUWAKUMBUSHA SHERIA ALIYOTUPA MUNGU - WAKRISTO WANAPASWA KUPENDANA."
"TUKIMPENDA MUNGU TUTAFANYA CHOCHOTE ATUAMBIACHO, NA AMETUAMBIA TUPENDANE."
"TAHADHARI NA VIONGOZI WAONGO WENGI WASIOAMINI YESU ALIKUJA ARDHINI KAMA BINADAMU NA MWILI KAMA WETU."
"WATU KAMA HAO WANAUPINGA UKWELI - NA KUMPINGA KRISTO."
"KAMA YEYOTE ATAKUJA KWAKO NA HAAMINI ALICHOFUNZA KRISTO, USIMUALIKE NYUMBANI KWAKO - AMA UTASHIRIKI KATIKA WOVU WAKE."[1]
[1] UKWELI LAZIMA UONGOZE ZOEZI LA KUPENDANA. UKWELI UNATHIBITISHA MIPAKA YA UPENDO NA UMOJA.
"TAHADHARI MSIWE KAMA WAO - HAKIKISHA MTAPATA TAJI KAMILI KUTOKA KWA BWANA."
KWELI...?
"UKITANGA NA KUPITA MAFUNZO YA KRISTO, UTAMUACHA MUNGU NYUMA."
"BALI KAMA U MUAMINIFU KWA MAFUNZO YA KRISTO UTAKUWA NAYE MUNGU PIA."
"KISHA UTAKUWA NA WOTE BABA NA MWANA."
"NINGEPENDA KUSEMA ZAIDI LAKINI SIO KATIKA BARUA HII KWANI NATUMAI KUJA KUWAONA HIVI KARIBUNI."


BARUA YA YOHANA YA TATU NA BINAFSI KWA ZOTE ILIANDIKWA KWA MTU JINA LAKE GAYO KUHUSU KUWA NA UKARIMU WA KIKRISTO KWA WAFANYAKAZI WA INJILI.
BARUA YA AWALI YA YOHANA ILIKUWA KUHUSU KUTOKUWA NA UKARIMU KWA WALIMU WAONGO - LAKINI BARUA HII INAHIMIZA UKARIMU KWA WALIMU WA KWELI WA INJILI.
MUAMINIFU DEMETRIO, TAFADHALI HAKIKISHA INAFIKISHWA KWA GAYO.
"MPENDWA GAYO, NAOMBA MWILI WAKO U MZIMA KAMA VILE ROHO YAKO ILIVYO."
"BAADHI YA NDUGU WAMENIPA FURAHA KWA KUNIAMBIA KUWA WANAISHI IKWA KIWANGO CHA INJILI."
"SIWEZI KUWA NA FURAHA ZAIDI KULIKO KUSIKIA MAMBO KAMA HAYA KUHUSU WANA WANGU."
"MNAFANYA KAZI YA MUNGU KWA KUWAANGALIA WALIMU WANAOSAFIRI NA MAMISHONARI - WAMEIAMBIA KANISA HAPA KUHUSU MATENDO YENU YA UPENDO."


"KWA SABABU HAWACHUKUI CHAKULA, MAVAZI, MAKAO WALA PESA KUTOKA KWA WASIOAMINI."
"INAFAA TUWAANGALIE ILI TUSAIDIANE KATIKA KAZI YA BWANA."
"NILITUMA BARUA FUPI HAPO AWALI, LAKINI DIOTREFE AKATAA KUNISIKIZA KWA MAJIVUNO YAKE."
KWA HIYO ADHANI HII NI KANISA YAKE! HATUTAMSIKIZA MZEE YULE MJINGA.
"HAKATAI TU KUWAKARIBISHA MAMISHONARI LAKINI PIA WENGINE WAKIWAKARIBISHA ANAWAFUKUZA KANISANI."
"MSIWACHE MFANO WAKE MBAYA UWAATHIRI - FUATA KILICHO CHEMA TU."
NA MNAWEZA KUMUAMBIA MZEE YULE MJINGA KUWAEKA MASKINI HAWA WATAKATIFU HAPA - TUNA WALIMU WETU.
WANAOFANYA KILICHO SAWA WANATHIBITISHA WA WANA WA MUNGU - NA WANAOENDELEA KWA WOVU WANATHIBITISHA SIO WA MUNGU.
NATUMAI KUWAONA HIVI KARIBUNI NA TUTAKUWA NA MENGI YA KUZUNGUMZA.
WAPENDWA HAPA WANATUMA SALAMU - TAFADHALI IPATIE KANISA SALAMU MAALUM KUTOKA KWANGU.


YUDA
YUDA ALIKUWA NDUGU WA KAMBO WA YESU KRISTO.
YESU ALIPOKUWA HAI ALIMKATAA KAMA MASSIAH - LAKINI BAADA YA KUFUFUKA AKAWA MFUASI WA KRISTO NA KIONGOZI WA KANISA LA KWANZA.
ALIKUWA AMEPANGA KUANDIKA KUHUSU WOKOVU LAKINI BADALA YAKE ALIANDIKA KUHUSU SHIDA KUBWA ZAIDI ILIYOIKUMBA KANISA - WALIMUA WAASI.
...SASA NAONA NI LAZIMA NIWAANDIKIE KUWASIHI KUUPIGANIA UKWELI AMBAO MUNGU ALITOA MARA MOJA KWA WATU WAKE WOTE KUWEKA BILA KUBADILISHA.
WALIMU WASIO WA KIUNGU WAMEPENYA NDANI - WAKISEMA TUNAWEZA KUFANYA CHOCHOTE TUNACHOKITAKA - BILA KUOGOPA ADHABU YA MUNGU.
MWISHO WAO USHAANDIKWA - KWANI WAMEGEUKA DHIDI YA MKUU WETU NA BWANA WA PEKEE YESU KRISTO.


"KUMBUKA UKWELI HUU - BWANA WALIOKOA TAIFA ZIMA KUTOKA NCHI YA MISRI KISHA AKAWAUA KILA MMOJA WAO AMBAYE HAKUMUAMINI NA KUMTII."
"NA MALAIKA WALIOTOKA KWAO - MUNGU AMEWAFUNGA NA MINYORORO KWA MAGEREZA YENYE GIZA - WANGOJA SIKU YA HUKUMU."
"MSISAHAU SODOMA NA GOMORA NA MIJI ILIYOKUWA KANDO KANDO WALIOJIPA KWA UASHERATI NA UPOTOSHAJI."
"WALIANGAMIZWA KWA MOTO - NA WAKO KAMA ONYO MPAKA WA LEO."


"WALIMU HAWA WAONGO WANAISHI MAISHA YASIYO NA MAADILI."
"WACHAFUA MIILI YAO NAO KUWACHEKA WALIO KATIKA MAMLAKA - HATA KUWADHIHAKI MALAIKA."
"LAKINI MIKAELI, MMOJA WA MALAIKA WAKUU ZAIDI, ALIPOSHINDANA NA IBILISI KUHUSU MWILI WA MUSA, HAKUMSHTAKI KWA KUMLAUMU."
MUNGU AKUKEMEE
"LAKINI WATU HAWA WANADHIHAKI NA KULAANI KITU CHOCHOTE WASICHOELEWA, NA KAMA WANYAMA, WANAFANYA WANACHOTAKA NA KUANGAMIZA ROHO ZAO."
YUDA 8-10


"OLE WAO! KWANI WANAFUATA MFANO WA KAINI ALIYEMUUA NDUGU YAKE."
"KAMA BAALAMU WATAFANYA CHOCHOTE KUPATA HELA."
"KAMA KORA HAWAKUMTII MUNGU NA WATAKUFA CHINI YA LAANA YAKE."
"WATU HAWA NI DOA KATIKA KARAMU ZA UPENDO ZA KANISA."
"NI KAMA MITUNDA BILA MATUNDA."
"AIBU YAO NA FEDHEHA NI KAMA POVU CHAFU LINALOBAKI UFUONI BAADA YA MAWIMBI MAKALI."
"WANATANGA KAMA NYOTA ZINAZONG'AA, LAKINI MUNGU AMEWATAYARISHIA WEUSI NA GIZA MILELE."


"HENOKO, ALIYEISHI VIZAZI SABA BAADA YA ADAMU ALIJUA KUWAHUSU WATU HAWA..."
TAZAMA BWANA AKIJA NA MAMILIONI YA WATAKATIFU WAKE.
"ATAWAKUSANYA WATU WA ULIMWENGI MBELE YAKE KWA HUKUMU, KUPEWA ADHABU NA KUTHIBITISHA MAOVU WALIYOYATENDA KWA KUMUASI MUNGU."
WATU HAWA WANAANZISHA UGOMVI NA WANAPENDA UOVU.
HAWANA ROHO MTAKATIFU NDNI YAO.
"WATU HAWA SIKU ZOTE WANALALAMIKA, KUFANYA WATAKACHO NA KUJIVUNA KWA MSHINDO."
"WANAONYESHA HESHIMA KAMA INAWAFAIDI PEKE YAKE."
LAKINI KUMBUKA WALIVYOSEMA MITUME WA BWANA YETU YESU KRISTO - KUWA WADHIHAKI HAWA WATAONEKANA SIKU ZA MWISHO NA WATAJIFURAHISHA KATIKA KILA NJIA YA UOVU INAYOWEZEKANA."

YUDA 14-19













SUPERBIBLE.TV